# Jinsi ya kukusanya sampuli ya mkojo wa katikati ya mkondo (MSU)

**Kwa watoto wakubwa, vijana na watu wazima wenye mfumo wa mkojo wa kike**

## Vipengele vya jumla

**Daima nawa mikono yako** kwa sabuni na maji kabla na baada ya kukusanya sampuli ya mkojo(mkojo).


**Usifungue kikopo kisicho na vijidudu** hadi utakapokuwa tayari kukusanya sampuli.

**Epuka kugusa sehemu ya ndani ya chombo cha kukusanyia mkojo**, na hakikisha sehemu zako za siri hazigusi sehemu yoyote ya chombo hicho

**Bandika lebo kwenye kikopo kabla ya kukusanya sampuli** ikiwa mtaalamu wako wa afya amekuomba kufanya hivyo.

## Ili kukusanya sampuli ya mkojo wa katikati ya mkondo

1



Ondoa kifuniko cha kikopo na ukiweke juu ya sehemu safi huku upande wa ndani ukiwa umeelekea juu.

2



Tumia mkono mmoja kutenganisha midomo ya uke (mikunjo ya ngozi inayozunguka tundu la uke) na uiweke ikiwa imetenganishwa.

3




Anza kukojoa kwenye choo (usikusanye mkojo wa mwanzo). Bila kusimamisha mtiririko wa mkojo, sogeza kikopo kwenye mkondo wa mkojo na ukusanye mkojo kiasi.

4



Jaza kikopo kwa mkojo mwingi kadiri wezekanavyo bila kuufanya umwagike, au hadi kwenye mstari wa alama ikiwa upo. Malizia kukojoa kwenye choo.

5



Rudisha kifuniko kwenye kikopo na ukikaze vizuri. Suuza na ukaushe sehemu ya nje ya kikopo ikiwa imelowa.

6



Peleka sampuli ya mkojo kwa mtoa huduma wako wa afya haraka iwezekanavyo, pamoja na fomu au lebo zozote ulizoombwa kujaza. Fuata vidokezo vilivyo kwenye ukurasa wa 2.

## Maelezo ya muhtasari

**Sampuli ya mkojo wa katikati ya mkondo ni nini?** Sampuli ya mkojo wa katikati ya mkondo ni mkojo unaokusanywa baada ya mkojo kuanza kutoka.

**Kwa nini ninahitaji kukusanya sampuli ya mkojo katikati ya mkondo?**
Mkojo unaotoka mwanzoni mwa mkondo wa mkojo unaweza kuchukua vijidudu kutoka kwenye ngozi, jambo ambalo linaweza kuathiri matokeo ya kipimo. Kukusanya sampuli katikati ya mkondo wa mkojo husaidia kuepuka hali hiyo na hutoa matokeo sahihi zaidi.

**Je, ninahitaji kuosha sehemu zangu za siri kabla ya kukusanya sampuli?**
Huhitaji kutumia vitambaa maalum vya kusafishia au bidhaa za kusafishia, isipokuwa kama mtaalamu wako wa afya atakuelekeza vinginevyo. Hakikisha tu eneo hilo ni safi na kavu.

**Je, ninaweza kutumia chupa au kikopo kutoka nyumbani?**
Unapaswa kutumia kikopo ambacho mtaalamu wako wa afya amekupa kwa ajili ya kukusanya sampuli.

**Je, ni muhimu ni lini ninakusanya sampuli?**
Jaribu kukusanya sampuli karibu iwezekanavyo na muda wa miadi yako ili kupata sampuli yenye ubora bora zaidi. Jaribu kukusanya sampuli kabla ya kuanza kutumia antibiotiki, ikiwa inawezekana.

**Je, kuna hali ambazo utaratibu huu unaweza kubadilika?**
Wakati mwingine mtoa huduma wako wa afya anaweza kupendekeza njia tofauti ya kukusanya sampuli ya mkojo. Ikiwa ni hivyo, fuata maelekezo watakayokupa.

## Vidokezo vya kuwasilisha sampuli ya mkojo

- **Wasilisha sampuli haraka.**
  Ipeleke kwa mtoa huduma wako wa afya haraka iwezekanavyo – ikiwezekana
  ndani ya saa mbili.

- **Angalia muda wa kuwasilisha sampuli.** Uliza muda wa mwisho -wa kuwasilisha sampuli, ili sampuli yako iweze kufika maabara siku hiyo hiyo.

- **Iweke katika hali ya baridi**
  Ikiwa huwezi kuwasilisha sampuli haraka, iweke kwenye mfuko wa plastiki na ihifadhi kwenye friji hadi utakapoweza kufanya hivyo.

- **Kutumia vikopo maalum visivyo na vijidudu**
  Baadhi ya vikopo vina unga wa kuhifadhi sampuli na alama ya kiwango cha kujaza. Jaribu kujaza hadi kwenye mstari wa alama, lakini ikiwa hu wezi, kusanya collect as much urine as you cantu kiasi kikubwa cha mkojo unachoweza.

**Changanua hapa** kwa maelezo zaidi.

© Hakimiliki ya Serikali ya Uingereza 2026. Toleo la 1. Imechapishwa: Julai 2026. Tarehe ya marekebisho: Julai 2029. Hati hii imetayarishwa kwa ushirikiano na wataalamu wa afya, wagonjwa na mashirika ya kitaalamu ya matibabu. TARGET inaendeshwa na Wakala wa Usalama wa Afya wa Uingereza.